BARAZA LA SANAA LA TAIFA



# MSANII

## TOLEO LA TISA

Sanaa ni Biashara, Uchumi na Ajira

+255 696466827
+255 740030595
+255 740030559

basata.tanzania

Majengo ya Utumishi, 18
Barabaraya,Kivukoni,
S.L.P.4779, Dar es Salaam.

# YALIYOMO

i. Kutoka kwa Katibu Mtendaji ....................................................02

ii. Je, Wajua kuwa Sanaa ni Zaidi ya Burudani.......................03

iii. Vipaji na Milango ya Mafanikio katika Sanaa................06

iv. Sekta ya Ubunifu na Ustawi wa Vijana............................08

v. Kutoka Kitaa Hadi Kimataifa.................................................10

vi. Mjue Msanii Wako...........................................................14

vii. Mdundo wa Taifa, Fursa ya Utambulisho na Ajira........16

viii. Muziki na Filamu za Vijana: Sauti ya Mabadiliko.........18

ix. BRELA na BASATA ...........................................................20

x. Uratibu wa Mashariki Creative Economy Expo 2025.....22

# Kutoka kwa Katibu Mtendaji

Kwa niaba ya Menejimenti na Watumishi wa **Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA),** tunayo furaha kukukaribisha katika Jarida la Msanii, Toleo la 09, linalotolewa kila baada ya miezi mitatu. Jarida hili ni chombo cha mawasiliano kinachotoa taarifa, miongozo, na mikakati kwa wadau wa sanaa nchini. Lengo lake ni kuhamasisha ubunifu, kuunganisha wasanii na wadau mbalimbali, na kuwa kielelezo cha kujenga uelewa wa sekta ya sanaa. Hii ni fursa ya kuwakaribisha wasanii karibu na Serikali, sekta binafsi, na asasi za kiraia.

Ninatumia fursa hii kuwakumbusha wasanii na wadau wote wa sanaa kujirasimisha kwenye Mfumo wa **BASATA** wa **Artist Management Information System (AMIS).** Usajili huu ni muhimu sana kwani unahakikisha haupotezi fursa za kipekee zinazotolewa na Serikali, wadau wa sanaa, na asasi zisizo za kiserikali. Ni njia ya kisheria na kitaalamu ya kuimarisha usimamizi wa vipaji, kushiriki kikamilifu katika shughuli za sekta ya sanaa, na kufaidika na mashirika yote yanayoshirikiana na BASATA.

Kupitia jarida hili, utapata taarifa sahihi, matukio muhimu, na mikakati ya kukuza na kuendeleza sanaa nchini. Lengo ni kusaidia wasanii na wadau wote wa sekta ya sanaa kupata maarifa muhimu, kuboresha vipaji, na kufahamu fursa zinazopatikana kupitia BASATA na wadau wengine.

BASATA inaendelea kushirikiana kwa karibu na wasanii, **taasisi za Serikali,** sekta binafsi, na wadau wa maendeleo ili kuhakikisha Sanaa inachangia kikamilifu katika maendeleo ya kiutamaduni, kijamii, na kiuchumi nchini. Ushirikiano huu unaimarisha tasnia ya sanaa na kutoa fursa zaidi kwa wasanii na wadau kushirikiana, kujifunza, na kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya sekta.

Karibu usome Jarida la Msanii, Toleo la 09 la **BASATA,** chombo chako cha kuaminika katika kuimarisha ustawi wa sanaa, kukuza vipaji, na kufanikisha fursa za maendeleo kwa wasanii na wadau wote wa sekta ya sanaa nchini Tanzania. Usajili na ushiriki wako ni muhimu ili kufaidika kikamilifu na fursa zinazotolewa na BASATA na wadau wake



**Bw. Edward E. Buganga.**

**Katibu Kaimu Mtendaji, BASATA**




## Je, Wajua kuwa Sanaa ni Zaidi ya Burudani

Hapo kale, sanaa ilionekana zaidi kama kipaji cha asili, chombo cha burudani, au sehemu ya kujifurahisha. Vijana na jamii walishirikiana kwenye michezo, ngoma za asili, uchoraji wa mila, na nyimbo za kienyeji kama sehemu ya tamaduni na sherehe. Lakini nyakati zimebadilika. Leo, sanaa si burudani pekee; ni biashara yenye thamani, ajira inayowapa vijana maisha bora, na chanzo kikubwa cha uchumi kwa taifa. Swali la kujiuliza ni hili: Je, wajua kwamba kipaji chako kinaweza kukulisha, kukuwezesha kuajiri wengine, na hata kuchangia pato la taifa?

Sanaa ikitazamwa kama biashara inabadilisha maisha. Muziki, uchoraji, fasheni, utunzi wa mashairi, filamu, ngoma za asili, na hata sanaa za kidigitali ni bidhaa zinazouzwa sokoni. Wasanii hujenga majina yao (brands), na kazi zao hubadilika kuwa bidhaa halisi. Mfano, Nandy ameweza kugeuza muziki wake kuwa biashara kubwa, kufungua duka la mitindo na kuandaa tamasha lake binafsi (Nandy Festival), ambalo linaajiri vijana wengi na kuingiza mapato makubwa. Hii ni ishara kwamba sanaa inapopewa mtazamo wa kibiashara, hubadilisha vipaji kuwa bidhaa, na msanii kuwa mjasiriamali.

Je wajua kuwa msanii mmoja anaweza kuajiri vijana zaidi ya kumi? Fikiria msanii wa muziki, ili kutoa kazi moja ya ubora, anahitaji mtayarishaji wa muziki, mpiga picha, mhariri wa video, meneja, mshauri wa mitandao ya kijamii, na wahasibu. Hawa wote hupata ajira kupitia kipaji cha msanii mmoja. Mfano, Frida Amani (rapa wa hip hop) amekuwa akishirikiana na wabunifu wa mavazi, wapiga picha na wanamitindo kujenga kazi zake. Kila kazi yake ni ajira kwa wengine. Vivyo hivyo, Walter Chilambo kwenye muziki wa injili hujumuisha waimbaji wa taustari, waandaaji wa sauti na washauri wa matangazo. Hii inathibitisha kuwa sanaa ni injini ya ajira.

Sanaa haimsaidii tu msanii binafsi bali pia taifa. Kazi za wasanii zinapouzwa, kodi inalipwa na hivyo kuongeza pato la taifa. Mashindano, matamasha na maonyesho ya sanaa huongeza mzunguko wa fedha kwenye jamii. Mfano, Mwasiti amekuwa akishirikiana na miradi ya kijamii na makampuni mbalimbali kupitia kampeni za kijamii.
Ushirikiano huu huleta manufaa si kwake tu bali pia kwa uchumi mpana wa kijamii. Vilevile, G Nako amefanikisha kipato kikubwa kupitia matangazo ya kibiashara na ushirikiano na makampuni makubwa.
Serikali, kupitia Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Bodi ya Filamu, COSOTA na Mfuko wa Utamaduni, ambazo zote ni taasisi za Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, imekuwa ikihimiza usajili wa kazi,

kulinda haki miliki, na kuwajengea uwezo wasanii kuona vipaji vyao kama biashara rasmi. Hatua hizi ni sehemu ya maono yanayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, yanayolenga kuhakikisha wasanii wanatambua thamani ya kazi zao na kufanikisha uwekezaji katika vipaji vyao.

Hii ni sehemu ya juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita kuhakikisha sanaa inakuwa nguzo thabiti ya uchumi wa taifa, ikichangia ajira, ukuaji wa biashara, na maendeleo endelevu ya sekta ya ubunifu, kwa mujibu wa dira ya kitaifa inayotaka vipaji vya vijana vitumike kikamilifu katika maendeleo ya taifa.

Mitandao ya kijamii imekuwa soko kubwa la kisasa kwa wasanii. Kupitia majukwaa kama YouTube, TikTok, Instagram, na mitandao mingine ya kidigitali, msanii anaweza kufikia mashabiki duniani kote bila gharama kubwa za usambazaji wa jadi. Mac Voice, kijana chipukizi kutoka lebo ya Next Level Music, ni mfano wa jinsi kizazi kipya kinavyotumia teknolojia kujitangaza na kupata mapato kupitia kazi zao.

Kazi za sanaa zinaweza kuuzwa kwa njia mbalimbali: muziki unaweza kusambazwa kupitia streaming na downloads, filamu na vipindi vya televisheni vinaweza kutolewa kwa majukwaa ya kidigitali, na bidhaa zinazohusiana na sanaa kama nguo, posters na vifaa vya burudani zinaweza kuuza moja kwa moja kwa mashabiki. Pia, ushirikiano na matangazo, maonyesho ya moja kwa moja, na vipindi vya utangazaji vya mtandaoni vinaongeza mapato kwa msanii.

Hii inaonyesha wazi kwamba kijana yeyote mwenye kipaji anaweza kuligeuza kuwa ajira na biashara kwa kutumia teknolojia kwa njia sahihi. Kipaji chako si tu burudani – ni fursa halisi ya kibiashara, chanzo cha mapato, na njia ya kuunda mustakabali wako wa kiuchumi.

Ni kweli kwamba sanaa inakumbana na changamoto kadhaa, zikiwemo upungufu wa mitaji, wizi wa kazi (piracy), mikataba mibovu na ukosefu wa elimu ya kibiashara. Changamoto hizi mara nyingi huweka vikwazo kwa wasanii, hasa vijana, kuendeleza vipaji vyao na kufanikisha biashara zao. Hapa ndipo kuarasimisha kazi zao kunapokuwa muhimu: Kusajili kazi ni njia ya kulinda haki miliki, kuhakikisha msanii anapata malipo sahihi, na kupunguza hatari ya kudanganywa katika mikataba.

Hata hivyo, haya siyo mwisho wa safari, wasanii wanaweza kushirikiana, kupata elimu ya ujasiriamali, kutumia vyema mitandao ya kijamii na kusajili kazi zao ili kulinda mali zao za kiakili. Aidha, Serikali na taasisi binafsi zinaendelea kutoa mafunzo, nafasi za mikopo, na msaada mwingine wa kifedha ili kuwasaidia vijana kufanikisha ndoto zao katika sekta ya ubunifu. Kwa kufanya hivyo, msanii anakuwa na udhibiti wa kazi zake, anapata fursa za biashara, na husaidia kuimarisha sekta ya sanaa kama nguzo ya uchumi wa taifa.

Mwana jamii, je, wajua kuwa sanaa si burudani pekee? Ni biashara inayouza bidhaa, ni ajira inayotoa nafasi kwa maelfu ya vijana, na ni uchumi unaoingiza pato kwa taifa. Sanaa inaweza kuwa njia ya kujiletea uhuru kifedha, kukuza vipaji vyako, na hata kuathiri jamii kwa njia chanya. Wakati umefika kwa vijana wa Kitanzania kuacha kuiona sanaa kama kipaji cha kujivunia tu, bali kama mtaji wa maisha, fursa ya kujenga jina na

umaarufu wa kitaifa na kimataifa. Sanaa ni Biashara; Sanaa ni Ajira; Sanaa ni Uchumi.

Thubutu leo kuligeuza kipaji chako kuwa chanzo cha mafanikio, changamoto na hata mradi unaoweza kubadilisha maisha yako na ya wengine. Usisubiri bahati, tengeneza fursa zako mwenyewe, uwe msanii aliye na malengo, mpiganaji wa ndoto zako na mtoaji wa thamani kwa jamii. Hii ndiyo safari ya kweli ya kutumia kipaji chako kufanikisha maisha na kuchangia maendeleo ya taifa.

Mwana jamii, je, wajua kuwa sanaa si burudani pekee? Ni biashara inayouza bidhaa, ni ajira inayotoa nafasi kwa maelfu ya vijana, na ni uchumi unaoingiza pato kwa taifa. Sanaa inaweza kuwa njia ya kujiletea uhuru kifedha, kukuza vipaji vyako, na hata kuathiri jamii kwa njia chanya. Wakati umefika kwa vijana wa Kitanzania kuacha kuiona sanaa kama kipaji cha kujivunia tu, bali kama mtaji wa maisha, fursa ya kujenga jina na umaarufu wa kitaifa na kimataifa. Sanaa ni Biashara; Sanaa ni Ajira; Sanaa ni Uchumi.

Thubutu leo kuligeuza kipaji chako kuwa chanzo cha mafanikio, changamoto na hata mradi unaoweza kubadilisha maisha yako na ya wengine. Usisubiri bahati, tengeneza fursa zako mwenyewe, uwe msanii aliye na malengo, mpiganaji wa ndoto zako na mtoaji wa thamani kwa jamii. Hii ndiyo safari ya kweli ya kutumia kipaji chako kufanikisha maisha na kuchangia maendeleo ya taifa.






## Vipaji na Milango ya Mafanikio katika Sanaa

Tangu enzi za kale, vipaji vimekuwa msingi wa ubunifu na maendeleo ya jamii. Watu walichora historia kwenye mawe ya Kondoa na kutumia ufundi wa mikono kutengeneza vyombo vya chakula na silaha za kujilinda. Baada ya uhuru wa Tanganyika mwaka 1961, vipaji vya vijana vilijionyesha kupitia muziki na Sanaa. Mfano mzuri ni wasanii wa maigizo waliotumia jukwaa kueleza changamoto za kijamii, au wachoraji waliobadilisha kuta za shule na majengo ya umma kuwa sehemu za elimu na mshikamano wa kijamii.

Kadri historia ilivyokwenda, vipaji vilianza kuonyesha nguvu za kipekee, ambapo katika enzi za ukoloni na baada ya uhuru, vijana walianza kutumia vipaji vyao katika Sanaa za muziki, uchoraji na ufundi wa kisasa. Mara nyingi vipaji hivi vilitumika pia kuelimisha, kuhamasisha na kuunda nafasi za kiuchumi.

Hadi leo, tunashuhudia vijana wakigeuza vipaji vyao kuwa ajira na biashara. Kuna wanaotumia uchoraji na ususi kutengeneza bidhaa za mikono zinazouzwa sokoni na mtandaoni. Wasanii wengine wanatumia muziki na mitandao ya kijamii kufikisha ujumbe wa kijamii, huku wengine wakitumia ujuzi wa teknolojia kubuni programu na majukwaa ya kidijitali. Mifano hii inaonyesha kwamba kuendeleza kipaji si kuongeza ujuzi pekee, bali ni kujijenga, kujiamini, na kutoa mchango chanya kwa jamii.

Kwa maneno mengine, kipaji ni kitu ambacho mtu ana asili ya kufanya vizuri kuliko watu wengine bila mafunzo au

kujifuza kwa muda mfupi. Mara nyingi kinajumuisha ubunifu, ufanisi na shauku. Kila mmoja wetu ana kipaji cha kipekee kama vile kuimba, kuandika, kuchora, kutengeneza vitu, au hata kuongoza. Changamoto iliyopo ni jinsi ya kugundua kipaji hicho na kukiendeleza hadi kuwa ujuzi halisi unaoweza kubadilisha maisha yako.

Kwanza, angalia yale unayopenda kufanya kwa hiari, kwa furaha bila kujisukuma. Tafiti za kitamaduni na za kisayansi zinaonyesha kuwa vipaji mara nyingi huonekana pale mtu anaposhiriki katika shughuli za kila siku, bila shinikizo. Njia nyingine za kugundua vipaji vyako ni pamoja. Angalia kazi au shughuli unazopenda na unazofanya kwa urahisi kuliko wengine. Vipimo vya ubunifu, akili, au stadi fulani vinaweza kukusaidia kutambua nguvu zako zilizofichika. Omba maoni kutoka kwa marafiki, walimu, au wenzako. Maoni yao yanaweza kufichua kipaji unachoweza kutoshughulikia peke yako.

Kutambua kipaji ni mwanzo tu; hatua inayofuata ni kukiendeleza. Shirikiana na mentors, wanakufundisha mbinu bora na kukuonyesha njia za kukua. Jihusishe kwenye mashindano, maonyesho, au miradi inayokupa changamoto. Kila jaribio ni fursa ya kujifunza na kuboresha kipaji chako. Mitandao ya kijamii na digital platforms ni njia nzuri ya kuonyesha kazi zako na kupata mrejesho kutoka duniani kote.

Kuendeleza vipaji ni zaidi ya kuongeza ujuzi; ni mchakato wa kujijenga binafsi na kuimarisha utu. Linapopandishwa vyema, kipaji huchochea motisha, kujiamini, na hutoa fursa ya kukabiliana na changamoto za maisha kwa ufanisi.

Vipaji vinavyopandishwa vinaweza kuwa msingi wa kujipatia kipato na kujenga heshima binafsi. Kwa njia hii, mtu anakuwa na uwezo wa kuchagua fursa zinazomfaa na kuunda mustakabali wake kwa uangalifu na busara. Zaidi ya faida binafsi, vipaji vilivyokuzwa vinachangia jamii kwa njia chanya. Vinasaidia kuendeleza mitindo bora ya kijamii, kuhamasisha wengine, na kutoa mchango wa kiutamaduni na kiuchumi unaoonekana na kuthaminiwa.

Inabidi kugundua kile unachokipenda kweli, kile kinachokufanya ujisikie mwenye furaha unachokifanya kwa hiari. Mara tu unapogundua kipaji hicho, tafuta njia za kukiendeleza, ama kujifunza kutoka kwa wataalamu, kushiriki kwenye mafunzo, au kujaribu mbinu mpya. Usiruhusu hofu, mashaka, au maneno ya wengine kukuzuia; changamoto ni sehemu ya safari ya ukuaji. Kila kipaji unachokiiendesha kwa bidii na shauku kinakuwa silaha yako ya kufanikisha maisha, kukuza ujuzi, na kuacha alama chanya katika jamii na ulimwengu kwa ujumla.





## Sekta ya Ubunifu na Ustawi wa Vijana

Sanaa si tu Burudani bali ni nguvu ya kubadilisha jamii, kiuchumi, na hata fikra za watu. Leo, tunaona vijana wa Tanzania wakijitokeza kama mabalozi wa mabadiliko katika sekta ya ubunifu, wakitumia vipaji vyao kuunda ajira, kuhamasisha jamii na kuleta maendeleo.

Vijana kama Diamond Platnumz, Harmonize na wengine wanathibitisha kuwa muziki unaweza kuunganisha mitaa na kimataifa. Kupitia majukwaa ya kidijitali na ushirikiano na wenzake wa kimataifa, wanaunda mitindo mipya na kutoa fursa kwa wenzake wachanga. Sauti zao si burudani tu, bali ni jukwaa la mawasiliano, elimu na biashara.

Vijana wa Tanzania wanaibuka katika michoro, picha, na sanaa za dijitali. Wasanii wanaonyesha hadithi za jamii, kuhamasisha wazo la ubunifu, na kuvutia wateja wa ndani na kimataifa. Hii inathibitisha kuwa sanaa ya visual inaweza kuwa kiungo cha maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Wazalishaji wa filamu kama Naeema Kassim wanatumia filamu kuzungumzia masuala ya kijamii kama elimu, haki za binadamu, na maisha ya mitaa. Filamu hizi hutoa fursa ya ajira na zinachangia kukuza uelewa wa jamii kuhusu changamoto na suluhisho.

Vijana wengi wanachanganya sanaa na teknolojia, kuunda muziki wa dijitali, video za 3D, michezo ya simu, na bidhaa nyingine za ubunifu. Hii inaonyesha kuwa sekta ya ubunifu si tu ya kuonyesha kipaji, bali ni ajira, biashara, na uchumi wa kweli.

Sanaa si tu Burudani bali ni nguvu ya kubadilisha jamii, kiuchumi, na hata fikra za watu. Leo, tunaona vijana wa Tanzania wakijitokeza kama mabalozi wa mabadiliko katika sekta ya ubunifu, wakitumia vipaji vyao kuunda ajira, kuhamasisha jamii na kuleta maendeleo.

Vijana kama Diamond Platnumz, Harmonize na wengine wanathibitisha kuwa muziki unaweza kuunganisha mitaa na kimataifa. Kupitia majukwaa ya kidijitali na ushirikiano na wenzake wa kimataifa, wanaunda mitindo mipya na kutoa fursa kwa wenzake wachanga. Sauti zao si burudani tu, bali ni jukwaa la mawasiliano, elimu na biashara.

Vijana wa Tanzania wanaibuka katika michoro, picha, na sanaa za dijitali. Wasanii wanaonyesha hadithi za jamii, kuhamasisha wazo la ubunifu, na kuvutia wateja wa ndani na kimataifa. Hii inathibitisha kuwa sanaa ya visual inaweza kuwa kiungo cha maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Wazalishaji wa filamu kama Naeema Kassim wanatumia filamu kuzungumzia masuala ya kijamii kama elimu, haki za binadamu, na maisha ya mitaa. Filamu hizi hutoa fursa ya ajira na zinachangia kukuza uelewa wa jamii kuhusu changamoto na suluhisho.

Vijana wengi wanachanganya sanaa na teknolojia, kuunda muziki wa dijitali, video za 3D, michezo ya simu, na bidhaa nyingine za ubunifu. Hii inaonyesha kuwa sekta ya ubunifu si tu ya kuonyesha kipaji, bali ni ajira, biashara, na uchumi wa kweli.



uchumi wa kweli.
Serikali ya Awamu ya Sita, kupitia BASATA, imeimarisha sekta ya ubunifu kwa kuanzisha mfumo wa urasimishaji wa kazi za sanaa (AMIS) unaorahisisha usajili, kulinda haki na kutoa fursa za kibiashara. Pia hutoa mafunzo na kuratibu maonesho ya kitaifa na kimataifa, yakisaidia vijana kufanikisha ndoto zao. Hatua hizi zinaonyesha dhamira ya Serikali kukuza vipaji na kuunda mazingira endelevu ya ubunifu. Vijana, kama chachu ya mabadiliko, wameweza kung'aa kimataifa huku sanaa ikiwa sauti ya kizazi kipya na daraja la mabadiliko. Anza safari yako leoweka ndoto zako kwenye hatua ya kwanza





## Kutoka Kitaa Hadi Kimataifa

Sanaa imekuwa daraja kubwa la maisha kwa vijana wengi waliokulia mitaani (ghetto). Mara nyingi, maisha ya ghetto hujaa changamoto za kiuchumi, kijamii na wakati mwingine hata kimaadili, ambapo vijana hukutana na vikwazo kama ukosefu wa ajira, mitazamo hasi kutoka kwa jamii, na mazingira magumu ya malezi. Hata hivyo, changamoto hizo hizo zimekuwa pia chemchemi ya ubunifu, msukumo wa uvumilivu na ari ya kupigania ndoto ambazo kwa macho ya wengi huonekana kama ngumu kutimia. Kwa vijana hawa, sanaa imekuwa kama mwanga unaowaongoza kutoka gizani, ikiwapa nafasi ya kueleza hisia zao, kueleza hadithi zao na kuonesha vipaji vilivyostawi katikati ya changamoto.

.

Leo, tunashuhudia vijana wengi waliokulia katika mitaa ya kawaida wakipenya na kuvunja mipaka ya ndani na ya kimataifa kupitia muziki, filamu, michezo ya kuigiza, uchoraji, mitindo ya mavazi na hata ubunifu wa kidijitali. Hadithi zao ni ushuhuda kwamba vipaji havizuiliwi na hali ya kiuchumi, bali vinahitaji malezi, kujituma na uthubutu wa kuamini katika ndoto. Ni vijana wanaobadilisha sura ya sanaa ya Afrika, wakiipa thamani na hadhi duniani kote, huku wakibaki kuwa mfano wa matumaini kwa vizazi vipya.

Nasibu Abdul Juma Issack, maarufu kama Diamond Platnumz. Yeye ni mfano halisi wa dhana ya “Kutoka Kitaa hadi Kimataifa”. Safari yake ya maisha ilianzia Tandale, Dar es Salaam, ambako alilelewa kwenye mazingira magumu yenye changamoto nyingi za kifedha. Akiwa kijana mdogo, alijitahidi kusaka riziki

kwa kuuza mitumba na kufanya vibarua vidogo vidogo huku akipigania ndoto yake ya muziki.

Kwa bidii, nidhamu na kutokata tamaa, Diamond alifanikiwa kupenya kwenye tasnia ya muziki wa Bongo Flava. Kazi yake ya kwanza kubwa iliyomtambulisha kwa umma ilikuwa "Kamwambie" (2009), ikifuatiwa na vibao kama "Mbagala" na "Nitarejea", ambavyo vilimfanya awe sauti mpya yenye mvuto katika anga za muziki wa Tanzania.

.Safari yake haikuishia hapo, Diamond alikuja kuwa mwanzilishi wa lebo ya WCB Wasafi, ambayo imetengeneza na kulea wasanii wakubwa kama Harmonize, Rayvanny, Zuchu na Lava Lava. Kupitia lebo hiyo, ameibadilisha tasnia ya muziki wa Afrika Mashariki kwa kuanzisha mfumo wa kitaalamu wa uzalishaji na usimamizi wa vipaji.

Kwa upande wa mafanikio ya kimataifa, Diamond amefanikisha kushirikiana na mastaa wa dunia kama Ne-Yo (kwenye "Marry You"), Rick Ross ("Waka"), Omarion ("African Beauty"), Morgan Heritage (Hallelujah), Ciara (Low) na hata kuonekana kwenye albamu ya Alicia Keys. Ushirikiano huu umepanua upeo wa muziki wa Bongo Flava na kuifanya Tanzania kutambulika kimataifa.

Mbali na muziki, Diamond amewekeza kwenye biashara ya vyombo vya habari kupitia Wasafi Media (radio na televisheni), na pia anatumika kama balozi wa chapa mbalimbali za kimataifa. Mafanikio yake yamemfanya kuwa mmoja wa wasanii wa Kiafrika wenye wafuasi wengi zaidi kwenye mitandao ya kijamii, na alitambulika pia kwenye

Kwa ujumla, Diamond Platnumz si tu msanii wa muziki bali pia ni nembo ya matumaini na uthubutu kwa vijana wa Afrika. Ameonesha kuwa mazingira magumu si kikwazo cha kufanikisha ndoto, na kwamba sanaa inaweza kuwa daraja la kutoka mitaani hadi kufikia majukwaa ya dunia.

Wapo wasanii wengi sana, lakini pia napenda kumuelezea Rajab Abdul Kahali, anayefahamika zaidi kwa jina la kisanii Harmonize au Konde Boy, mzaliwa wa Kijiji cha Chitoholi Wilaya ya Tandahimba Mkoani Mtwara, kusini mwa Tanzania. Safari yake ya muziki ni simulizi ya uthubutu na uvumilivu.

Akiwa kijana mdogo, Harmonize alianza kupenda muziki lakini hakupokelewa kirahisi. Mara nyingi alikataliwa kwenye studio na hata alipojaribu kushiriki katika matamasha madogo yanayoibua Vipaji kama vile BSS hakupata nafasi ya kuthibitisha kipaji chake. Hata hivyo, hakukata tamaa kama alivyokuja kusisitiza Katika Wimbo wake wa "never give up" aliendelea kupambana hadi alipochukuliwa na Diamond Platnumz kupitia lebo ya WCB Wasafi mnamo mwaka 2015.

Kupitia WCB, Harmonize aling'aa kwa mara ya kwanza kupitia wimbo "Aiyola", uliomfungulia milango ya umaarufu Tanzania na Afrika Mashariki. Baadaye akatoa vibao maarufu kama "Kwa Ngwaru" (akiwa na Diamond), "Happy Birthday", na "Bado", ambavyo vilimtambulisha kama sauti mpya yenye mvuto katika Bongo Flava.

Baada ya kujijengea jina, Harmonize aliamua kuanzisha lebo yake binafsi ya Konde Gang (Konde Music Worldwide) mwaka 2019, akiamini katika kujitegemea na kukuza vipaji vipya. Kupitia lebo hiyo, amefanya kazi na wasanii chipukizi na kusimama kama mfano wa msanii aliyejitengenezea njia yake.

Kimataifa, Harmonize ameshirikiana na mastaa kama Diamond Platnumz ("Kwa Ngwaru"), Burnaboy ("Kainama"), Mr Eazi, na Spice Diana kutoka Uganda. Nyimbo zake zimekuwa zikichezwa ndani na nje ya Afrika, zikimpa nafasi ya kushiriki katika matamasha makubwa.

Leo, Harmonize anatambulika si tu kama msanii wa Bongo Flava, bali pia kama kiongozi wa kizazi kipya cha muziki Tanzania. Ametumia changamoto alizopitia kama ngazi ya kujijenga, na anaendelea kuwa msukumo kwa vijana wengi wanaoamini kuwa ndoto zinaweza kufikiwa kupitia bidii, nidhamu na uvumilivu.

Vilevile, yupo msanii Rayvanny, ambaye jina lake halisi ni Raymond Shaban Mwakyusa, alianza safari yake ya muziki kutoka mkoani Mwanza. Alikua akiwa na ndoto kubwa za muziki ingawa hakuwahi kuwa na mtaji wa kutosha. Hii haikumzuia kutumia kipaji chake cha asili na uthubutu, kujipatia nafasi kupitia mashindano ya muziki na matangazo ya mtandaoni.

Safari yake ilipata mwanga zaidi alipokuwa mwanachama wa lebo ya WCB Wasafi ya Diamond Platnumz, ambapo alipata fursa ya kushirikiana na wasanii wenzake na kupanua mtandao wake wa muziki. Mwaka 2017, juhudi zake zilianza kuzaa matunda alipoibuka mshindi wa BET International Viewers' Choice Award, akitambulika kimataifa kama sauti mpya ya Tanzania.

Rayvanny pia amejitahidi kuunda alama yake binafsi, akianzisha lebo yake ya "Next Level Music" (NLM), ikimruhusu kushirikiana na wasanii mbalimbali wa kimataifa kama Khaligraph Jones (Kenya) na Lino (Tanzania). Nyimbo zake maarufu kama "Tetema" na "Kwetu" zimekuwa nguzo ya kizazi cha vijana, zikionyesha mchanganyiko wa muziki wa asili wa Tanzania na mitindo ya kimataifa. Kupitia safari hii, Rayvanny amekuwa mfano wa jinsi kipaji, uvumilivu na mkakati unaoelekezwa kimfumo unaweza kumfanya msanii kutoka mitaa ya kawaida kufikia vikao vya kimataifa.

Wapo pia wasanii wengi wa nje kwa kutambua wachache ambao ni Burna Boy alikulia katika mtaa wa Port Harcourt, Nigeria. Muziki kwake ulikuwa njia ya kueleza maisha ya vijana wa Kiafrika waliokutana na changamoto nyingi. Alianza taratibu, lakini leo hii amekuwa bingwa wa Grammy na msanii anayefanya maonyesho makubwa barani Ulaya, Marekani na Asia. Muziki wake wa Afro-fusion ni mfano wa namna ghetto linavyoweza kutoa sauti ya dunia.

Aidha, Davido ambaye ni Mnaijeria, ingawa anatoka familia yenye uwezo, Davido aliamua kujijengea jina kupitia ujuzi na muziki wake. Alianza mitaani akifanya kazi na vijana wa kawaida, na akajenga mashabiki waliomfikisha kimataifa. Hadithi yake inadhihirisha kuwa hata kijana wa ghetto anaweza kushirikiana na mtu mkubwa, na wote wakainua bendera ya Afrika.

Kwanini tunasema kutoka ghetto hadi kimataifa, ni kwasababu wasanii hawa wamekuwa kama kioo Katika kukuza sekta ya muziki kiuchumi, kushiriki matamasha ya kimataifa na kubadilisha mpangilio wa malipo kwenye matamasha wanayoalikwa kitaifa na kimataifa kutoka Fedha ya kawaida hadi kufikia milioni 200 kwa tamasha moja, hali hii imeweza kubadilisha Mfumo wa Maisha yao unaowawezesha kulinda chapa zao na Kutoa ajira kwa vijana.

Hadithi hizi za vijana wasanii waliotoka ghetto hadi Kimataifa ni kioo cha matumaini kwa kizazi kipya. Zinathibitisha kuwa sanaa ni zaidi ya burudani; ni daraja la kubadili maisha, kuinua jamii na kuipa Afrika sauti yenye heshima duniani.





# Mjue Msanii Wako

## Mwanamuziki wa Hip Hop; Kutoka Tanga Hadi Umaarufu Afrika Mashariki

### Utangulizi
William Nicholaus Lyimo, anayejulikana zaidi kwa jina la kisanii Bill Nass, ni msanii wa muziki wa hip hop kutoka Tanzania aliyezaliwa tarehe 11 Aprili 1993 katika Mkoa wa Tanga. Msanii huyu mwenye asili ya Kichagga amejijengea heshima kubwa ndani na nje ya Tanzania kupitia vipaji vyake vya muziki, ubunifu na ushawishi mkubwa katika jamii ya vijana. Mnamo mwaka 2017, kituo cha kimataifa cha MTV Base kilimtaja miongoni mwa wasanii "50 Artists To Watch For" jambo lililomweka kwenye ramani ya kimataifa. Hadi sasa, Bill Nass anaendelea kuwa miongoni mwa nyota wakubwa wa muziki wa kizazi kipya nchini na barani Afrika.

### Maisha ya Awali na Elimu
Bill Nass alizaliwa katika Hospitali ya Bombo, Tanga na wazazi wake ni wenyeji wa Mkoa wa Kilimanjaro. Safari yake ya elimu ilianzia Shule ya Msingi Mbuyuni (2000–2003), kisha Shule ya Msingi Mkunguni jijini Dar es Salaam. Alisoma Katika Sekondari ya Oysterbay (2007–2010), kisha kuendelea na masomo ya juu katika Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) ambapo alihitimu Shahada ya Ununuzi na Ugavi (2017).

### Safari ya Muziki
Bill Nass alianza kupata umaarufu mwaka 2014 baada ya kuachia wimbo wake wa kwanza "Raha". Mwaka uliofuata, aliteuliwa kwenye Kilimanjaro Tanzania Music Awards (KTMA 2015) kama msanii bora chipukizi.
Mwaka 2017 ulikuwa wa kipekee kwake baada ya kushiriki katika Coke Studio Africa kama msanii wa "Big Breakthrough Artist" ambapo alitumbuiza pamoja na wasanii kutoka Uganda na Ethiopia. Aidha, ameshiriki kwenye majukwaa makubwa ya muziki nchini ikiwemo Fiesta na Wasafi Festival.

Mwaka 2021, Bill Nass alianzisha Mafioso Inc., lebo yake ya muziki na kufanikiwa kutoa ngoma zilizotikisa kama "Puuh" akimshirikisha Jay Melody, wimbo ulioongoza chati za Boomplay kwa wiki sita mfululizo na kuvunja rekodi kwa zaidi ya milioni 51 za wasikilizaji mtandaoni.

Mnamo 2022, alinyakua tuzo ya Msanii Bora wa Hip Hop (Tanzania Music Awards) na mwaka 2025 akatangazwa Msanii Bora wa Hip Hop Afrika Mashariki (EAEA Awards) akiwashinda wanamuziki wakubwa kutoka Kenya, Uganda na Rwanda.

Mradi wa Kijamii: Chuo kwa Chuo
Mwaka 2024, Bill Nass alizindua kampeni ya vijana iitwayo "Chuo kwa Chuo". Mradi huu ulijikita katika kutembelea vyuo na taasisi mbalimbali nchini kwa ajili ya burudani, mashindano ya vipaji na mijadala ya kielimu kuhusu masuala ya afya ya akili na ujasiriamali.

Licha ya changamoto ndogo zilizojitokeza, ikiwemo mjadala mkali baada ya tukio katika Chuo cha TIA Dar es Salaam, mpango huu ulipongezwa kwa ubunifu na mchango wake katika kuwaunganisha vijana kupitia muziki, elimu na utamaduni.

## Maisha Binafsi

Majina halisi ya Bill Nass na majina halisi ya Faustina Charles Mfinanga (Nandy). Wawili hawa ni baadhi ya wasanii maarufu wa muziki wa Bongo Fleva nchini Tanzania, na safari yao ya maisha binafsi imekuwa ikifuatiliwa kwa karibu na mashabiki kutokana na uhusiano wao wa kimapenzi.Mwaka 2020, uhusiano wao ulionekana kuwa thabiti zaidi na walianza kushirikiana kwa karibu zaidi katika maisha binafsi na kazi zao za kisanii. Baada ya kipindi cha uhusiano wa kudumu na mshikamano thabiti, waliufanya uhusiano wao rasmi kwa kufunga ndoa mwaka 2022. Hadi sasa, wanajulikana kuwa na mtoto mmoja na wakiwa mstari wa mbele katika muziki wa Tanzania, wanasalia mfano wa mshikamano, upendo na ushirikiano wa kisanii.

Mbali na muziki, Billnass ametumia taaluma yake ya Biashara kutoka CBE kuanzisha kampuni ya vifaa vya kielektroniki, Nenga Tronix, mwaka 2021. Kampuni hii inauza bidhaa za kisasa kama simu, kompyuta na vifaa vya nyumbani, kwa lengo la kutoa huduma bora, bidhaa zenye ubora na bei nafuu, sambamba na kukuza ajira kupitia ujasiriamali.

## Tuzo na Mafanikio

(i) KTMA 2015 – Msanii Bora Chipukizi (nominated)
(ii) Tanzania Music Awards 2022 – Msanii Bora wa Hip Hop
(iii) EAEA Awards 2025 – Msanii Bora wa Hip Hop Afrika Mashariki

Kwa zaidi ya muongo mmoja, Bill Nass ameendelea kuwa chachu ya maendeleo ya muziki wa hip hop nchini Tanzania. Uwezo wake wa kuunganisha muziki, elimu, na uhamasishaji wa kijamii umemfanya kuwa mfano bora wa kuigwa na vijana wengi. Kupitia kazi zake na miradi yake ya kijamii, amethibitisha kuwa sanaa ni zaidi ya Burudani ni chombo cha mabadiliko, biashara, na daraja la kuunganisha jamii.






# Mdundo wa Taifa, Fursa ya Utambulisho na Ajira

## Mwanamuziki wa Hip Hop; Kutoka Tanga Hadi Umaarufu Afrika Mashariki

**Utangulizi**

Singeli imeendelea kujipatia mashiko makubwa ndani na nje ya mipaka ya Tanzania kutokana na kasi yake, ubunifu na ujumbe unaogusa maisha ya vijana na jamii kwa ujumla. Kutokana na umaarufu huo unaoongezeka, pendekezo la Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mheshimiwa Prof. Paramagamba Kabudi la kuifanya Singeli kuwa alama na utambulisho wa Tanzania duniani linaonekana kuwa na mashiko makubwa. Muziki huu una ladha ya kipekee inayochota kutoka kwenye maisha ya kila siku ya Watanzania, jambo linaloweza kuipa Tanzania nafasi ya kipekee kimataifa kupitia sanaa.

Kwa muda mrefu muziki wa kizazi kipya nchini Tanzania, hususani Bongo Fleva, umeendelea kujizolea umaarufu mkubwa ndani na nje ya mipaka yetu. Hata hivyo, licha ya mafanikio hayo, mjadala mkubwa umekuwa ukijitokeza juu ya namna muziki huu unavyopoteza alama yake ya kipekee kwa sababu ya kuiga mitindo kutoka nje ya nchi.

Mitindo hiyo ni kama vile hip hop ya Marekani, rumba ya Kongo, afrobeat ya Nigeria na hata mitindo ya Kiafrika kama Kwaito na Amapiano. Upungufu huu unatufanya tuonekane kama tunafuata badala ya kuongoza. Ndipo Singeli ikazaliwa ambayo ni sauti ya mitaa, hadithi za wananchi, na sasa ni sehemu ya urithi wetu wa Taifa.

Singeli ni muziki wa kisasa uliochipukia Pwani ya Tanzania na kuenea kwa kasi jijini Dar es Salaam kisha maeneo mengine nchini. Ni muunganiko wa mitindo ya Taarab, Bongo Fleva,

Hii ni kuanzia wasanii, watayarishaji, waongozaji wa video, hadi wamiliki wa majukwaa ya burudani. Ndiyo maana Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Bodi ya Filamu, Bodi ya Utalii na Wizara zinazoshughulika na sanaa na utamaduni wanapaswa kushirikiana ili kuuweka Singeli kwenye ramani ya dunia.

Licha ya kupaa kwake, Singeli inakabiliana na changamoto kadhaa, kama vile ukosefu wa miundombinu na rasilimali za kurekodi na kusambaza muziki kwa ubora wa kimataifa. Video na nyimbo nyingi hutengenezwa kwa bajeti ndogo, jambo linalowafanya wasanii washindwe kuingia kwenye ushindani wa kimataifa. Ukosefu wa elimu ya biashara ya muziki na hakimiliki kwa wasanii chipukizi. Kutokana na wasanii wengi "kutoendana na viwango," taifa limeanza kuwawekea mazingira bora ya mafunzo, fursa na uwezeshaji.

Katika hatua kubwa ya kihistoria, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo imetangaza kwamba Singeli imeorodheshwa rasmi kama moja ya Urithi wa Utamaduni Usioshikika wa Tanzania, hatua inayoupa nafasi kuorodheshwa na UNESCO. Akizungumza jijini Dar es Salaam, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara, Methusela Ntonda, alieleza: "Singeli si muziki wa kuburudisha tu, bali ni nyenzo ya ajira, mshikamano wa kijamii na alama ya utambulisho wa taifa. Ndiyo maana tunauchukua kama mdundo rasmi wa taifa letu." Kwa sasa Singeli limeunganishwa na vipengele vingine vya urithi kama michoro ya Tingatinga, sanaa za Kimakonde, taarab, tambiko la Waluguru, tamasha la Mwakakogwa, tamasha la Bulabo, ngoma ya Msewe na hata kilimo cha kontua cha Mbinga Ruvuma.

Singeli si tu muziki wa kasi, bali ni mwale wa utambulisho wa Watanzania. Ni sauti inayoweza kuutangaza utamaduni wetu duniani na kuwa injini ya maendeleo ya vijana. Hatua ya serikali kuutambua kama mdundo wa taifa ni uthibitisho kwamba Singeli sasa si burudani ya mitaa pekee, bali urithi unaohitaji kuenziwa, kulindwa na kuendelezwa.





## Muziki na Filamu za Vijana: Sauti ya Mabadiliko

**Utangulizi**
Tanzania ina historia ndefu na tajiri ya muziki na filamu, ambayo imekuwa sehemu ya maisha ya kila siku ya jamii. Kuanzia enzi za ngoma za asili na simulizi za jadi zilizokuwa zikisimuliwa usiku kuzunguka moto, sanaa imekuwa chombo cha mawasiliano, urithi na mshikamano wa kijamii. Miaka ya 1960 na 1970, muziki wa dansi na taarab ulitawala, ukiwa kioo cha jamii na sauti ya kisiasa katika enzi ya uhuru. Kadiri muda ulivyopita, vijana walianza kuibuka na mitindo mipya ya muziki kama Bongo Flava, ambayo ilizaliwa mwishoni mwa miaka ya 1990 na kuwa ishara ya utambulisho wa kizazi kipya.

Kwa kizazi cha sasa, muziki na filamu si burudani pekee, bali ni jukwaa lenye nguvu la mawasiliano na mabadiliko ya kijamii. Vijana wanavitumia kama njia ya kueleza hisia, kuibua mijadala, na kutoa suluhisho kuhusu changamoto zinazowakabili. Kupitia nyimbo na filamu, mada muhimu kama ukosefu wa ajira, ufisadi, mapenzi yenye heshima, usawa wa kijinsia, na amani huwasilishwa kwa lugha rahisi na inayoeleweka na jamii.

Kwa mfano, msanii Zuchu amekuwa akitumia muziki wake kuzungumzia nafasi ya wanawake na mapenzi yenye heshima, huku akiwahamasisha vijana kujiamini na kuendeleza vipaji vyao. Vilevile, kupitia filamu, Elizabeth Michael (Lulu Diva) ameonesha namna maamuzi mabaya yanavyoweza kuathiri maisha ya kijana, lakini pia akibainisha uwezekano wa kubadilika na kujifunza kutokana na makosa.

Muziki na filamu vina uwezo wa kufikia hadhira kubwa zaidi kuliko vyombo vingi vya habari. Vijana wanapopeleka ujumbe wao kupitia sanaa, ujumbe huo unavuka mipaka ya kijiografia na kijamii, ukafika kwa watu wa rika na tamaduni

tofauti. Hii inafanya sanaa kuwa chombo chenye nguvu ya mawasiliano na ushawishi mkubwa. Nyimbo zinazozungumzia amani, mshikamano, na maendeleo zimekuwa chombo cha kulinda mshikikano wa taifa. Kwa kupitia mashairi, midundo, na maneno yenye maana, wasanii huchangia katika kuhamasisha misukosuko chanya, kupunguza migawanyiko, na kuhimiza mshikamano wa kijamii. Hii ni muhimu hasa katika kuimarisha utamaduni wa mshikamano na ushirikiano kati ya wananchi.

Filamu pia zimekuwa dira ya mabadiliko ya tabia na mtazamo. Zinapogusa changamoto za familia, elimu, afya, au maadili, filamu hutoa mfano halisi unaoeleweka na kuamsha fikra za wananchi. Hii inachangia katika mabadiliko chanya ya jamii, kwani hadhira inapoona hali halisi, inakuwa na motisha ya kuchukua hatua za kuboresha maisha yao na jamii zao.

Historia ya muziki na filamu nchini Tanzania inaonyesha wazi kwamba sanaa si burudani tu, bali ni urithi wa kitamaduni, zana ya elimu, na sauti yenye nguvu ya mabadiliko. Kutoka kwenye ngoma za asili, taarab, bongo fleva hadi filamu za kisasa, wasanii wametumia vipaji vyao kuwasilisha ujumbe wa kijamii na kuendeleza utamaduni wa taifa.

Vijana wa kizazi hiki wamechukua urithi huu na kuubadilisha kuwa jukwaa la kuhamasisha jamii, kufundisha maadili, na kuunganisha wananchi. Nyimbo na filamu zao huchochea mijadala kuhusu amani, mshikamano, maendeleo, na haki za kijamii, huku wakiwahimiza wenzao kushiriki katika mabadiliko chanya.
Hakika, “Sanaa ni Sauti Yetu.” Kupitia muziki na filamu, vijana wanaendelea kuandika simulizi za matumaini, mshikamano, na maendeleo ya taifa. Kila wimbo na kila filamu ni hatua ya kuimarisha mshikikano wa kijamii na kuchangia katika kufanikisha mustakabali bora wa vijana na taifa kwa ujumla.






# BRELA na BASATA Wasaini Makubaliano ya TEHAMA kwa Maendeleo ya Sanaa.

Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), ni taasisi ya Serikali chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, yenye jukumu la kusimamia, kukuza na kuendeleza sanaa nchini Tanzania. Pia inahakikisha wasanii na kazi za sanaa zinasajiliwa, kulindwa na kufuata maadili. Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), ni wakala wa Serikali ulio chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara, wenye jukumu la kusajili biashara, kampuni, alama za biashara (trade/service marks), pamoja na kutoa leseni. Pia, unahakikisha mazingira ya kisheria na kibiashara yanaimarishwa ili kuchochea maendeleo ya uchumi. Katika kuimarisha msingi wa mikakati ya kukuza sekta ya sanaa na ubunifu kama chachu ya maendeleo ya uchumi Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) na Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) wametia saini hati ya makubaliano ya ushirikiano kupitia mifumo ya TEHAMA. Hatua hii inalenga kuimarisha ushirikiano wa taasisi hizi mbili katika urahisishaji wa huduma, ukusanyaji wa takwimu sahihi na kuongeza uwazi na uwajibikaji kwa wadau wa sekta ya sanaa na ubunifu.

Makubaliano haya pia yamezingatia agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, linalohimiza mifumo ya kielektroniki ya Serikali kusomana ili kuongeza ufanisi, kupunguza urudufu wa kazi, na kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora kwa haraka na kwa gharama nafuu. Tukio hili limefanyika leo, tarehe 12 Agosti 2025, katika ukumbi wa mikutano wa BRELA, Dar es Salaam, na linatazamwa kama hatua muhimu ya kuimarisha mchango wa sekta ya sanaa na ubunifu katika uchumi wa taifa.

Makubaliano haya yanalenga kurahisisha na kuimarisha mawasiliano na utoaji wa huduma baina ya taasisi hizi mbili,

hususan katika usajili na utoaji wa vibali kwa wasanii na vikundi vya sanaa nchini. Hatua hii inalenga pia kuondoa urasimu, kuongeza ufanisi, na kuhakikisha uwazi katika upatikanaji wa huduma kwa wadau wa sanaa. Kwa mujibu wa takwimu kutoka Kitengo cha Usajili cha BASATA, zaidi ya vikundi 400 vya sanaa vimesajiliwa na kupatiwa vibali kupitia mfumo wa AMIS (Artists Management Information System), ambao umeunganishwa na mfumo wa BRELA wa usajili wa biashara na makampuni (ORS). Ushirikiano huu unatarajiwa kuongeza idadi ya wasanii na vikundi vitakavyonufaika, kuimarisha uhifadhi wa takwimu na taarifa sahihi, pamoja na kuwezesha Serikali kupanga na kutekeleza sera za kukuza sekta ya sanaa na ubunifu kwa ufanisi mkubwa zaidi.

Akizungumza katika hafla hiyo, Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa, amesema makubaliano hayo ni hatua muhimu ya kuimarisha huduma kwa wateja kwa njia ya kisasa na yenye ufanisi: "Makubaliano haya yanalenga kuunganisha mifumo ya TEHAMA ili kurahisisha huduma kwa wateja popote walipo, kudhibiti matumizi sahihi ya taarifa, na kuzuia upotoshaji wa taarifa. Hii ni sehemu ya utekelezaji wa maagizo ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha mifumo ya kielektroniki ya Serikali inasomana ili kuongeza ufanisi wa huduma."

Kwa upande wake, Katibu Mtendaji wa BASATA, Dkt. Kedmon Mapana, amesema ushirikiano huo utaongeza ufanisi wa usajili wa wasanii na vikundi vyao: "Ushirikiano huu utaondoa urasimu, kuimarisha ubora wa taarifa za usajili, na kuwezesha




wasanii kujisajili kwa urahisi zaidi. Pia utasaidia kuondoa changamoto za kisheria zinazotokana na upungufu wa taarifa au usahihi wake."

Taasisi hizi mbili zina jukumu muhimu katika kuratibu na kusimamia kazi za sanaa na biashara nchini: BASATA ikihusika moja kwa moja na usajili na utoaji wa vibali kwa wasanii na vikundi vya sanaa, na BRELA ikiwa na jukumu la usajili wa biashara na utoaji wa leseni. Kupitia makubaliano haya, ushirikiano wao utaimarisha mawasiliano ya ndani, ukaguzi wa ubora, na urasimishaji wa kazi za sanaa na biashara nchini, kwa manufaa ya taifa na wadau wote wa sekta ya sanaa.






## BASATA Yajivunia Uratibu wa Mashariki Creative Economy Expo 2025

Serikali kupitia Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), ikishirikiana na wadau mbalimbali wa sekta ya ubunifu, imefanikisha kwa kiwango cha juu uratibu wa Mashariki Creative Economy Expo 2025. Tukio hili kubwa lililofanyika katika ukumbi wa Mlimani City, Dar es Salaam tarehe 14 – 16 Agosti 2025. EXPO hii imekuwa jukwaa muhimu la kuonesha bidhaa bunifu, kujenga mitandao ya kibiashara na kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa.

Ushirikiano wa BASATA na wadau umeonesha dhamira ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kukuza sekta ya ubunifu kama nguzo ya uchumi, ajira na utambulisho lililoandaliwa na Culture and Development East Africa (CDEA) kwa ushirikiano na BASATA, Bodi ya Filamu Tanzania na COSOTA, liliwakutanisha zaidi ya washiriki 2,000 kutoka Tanzania na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mgeni rasmi alikuwa Dkt. Emmanuel Ishengoma, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Sanaa, aliyesisitiza dhamira ya serikali kushirikiana na wadau kukuza uchumi wa ubunifu na fursa za ajira. BASATA kupitia viongozi wake walibainisha kuwa ushirikiano kati ya serikali, sekta binafsi na wabunifu utachochea mchango wa sanaa katika pato la taifa.

Mafanikio ya EXPO yalihusisha maonesho ya bidhaa na huduma zaidi ya 150 kutoka kwa wabunifu wa ndani na nje ya nchi, pamoja na majadiliano ya kitaalamu yaliyojumuisha wataalamu 15 wa kimataifa. Pia kulifanyika warsha na madarasa ya kukuza ujuzi wa wabunifu wachanga na wazoefu katika masoko, matumizi ya teknolojia na usimamizi wa




mapya na kuchochea ukuaji wa uchumi wa ubunifu.

Kupitia tukio hili, Tanzania imeimarisha nafasi yake kama kitovu cha ubunifu Afrika Mashariki na kuongeza mwonekano wake kimataifa, sambamba na utekelezaji wa Mkataba wa African Continental Free Trade Area (AfCFTA). EXPO pia imeimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa, sera za ubunifu na mnyororo mzima wa thamani wa sekta ya sanaa.

Mashariki Creative Economy Expo 2025 imeonyesha kuwa ushirikiano kati ya BASATA, serikali na wadau binafsi ni msingi thabiti wa kukuza sekta ya ubunifu, kuongeza ajira kwa vijana, na kuinua thamani ya kazi za wabunifu ndani na nje ya nchi.




Mashariki
Creative Economy
EXPO'25

BARAZA LA SANAA LA TAIFA-BASATA

NATIONAL ARTS COUNCIL

Sanaa ni Biashara, Uchumi na Ajira

+255 696466827
+255 740030595
+255 740030559

basata.tanzania

Majengo ya Utumishi, 18
Barabaraya,Kivukoni,
S.L.P.4779, Dar es Salaam.